**TAARIFA MAALUM KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSIANA NA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA KUPIGA VITA MATUMIZI NA BIASHARA HARAMU YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI.**

**<u>TAREHE: 25 JUNI, 2023.</u>**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na mabwana**

**Assalamu Aleykum,**

Awali ya yote kumshukuru Mwenyenzi Mungu muumba mbingu na ardhi na mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima pamoja na afya njema kukutana siku ya leo na kutoa taarifa ya kupiga marufuku ya matumizi ya Dawa za Kulevya.

**Ndugu Wananchi,**

Kila mwaka ifikapo tarehe 26 Juni dunia nzima tunaungana pamoja kuadhimisha Siku ya Kupiga Vita Kilimo, Matumzi, Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya Duniani (**International Day Against Drug Abuse and Illicit Trafficking**). Maadhimisho haya ni kufuatia Azimio Nambari 42/112 la Baraza Kuu la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNO) lililopitishwa Disemba 1987. Azimio hilo linataka mataifa wanachama wa UNO kuifanya tarehe 26 juni kuwa ni siku maalum ya kupiga vita biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya duniani. Chini ya Azimio hilo Baraza liliagiza kuwa siku hii iratibiwe na kuandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani yaani (**United Nations Office on Drugs**

**and Crimes – UNODC**) lenye makao makuu yake huko **Geneva, Switzerland**.

**Ndugu Wananchi,**

Historia ya siku hii ya kupiga vita kilimo, usafirishaji, biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya duniani ni ndefu na siyo ya jana wala juzi. Uthibitisho wa hayo ni kutajwa na kuharamishwa kwa kilimo na matumizi yake katika maandiko yote vitabu vitakatifu vya dini zote.

Aidha, Taarifa zilizopo ni kuwa wapiganaji wa **Vita Kuu ya Pili ya Dunia (1939-1945)** walikuwa wakipewa na kutumia baadhi ya dawa hizo hasa bangi ili kuwaliwaza kwa machofu ya vita hiyo waweze kupata nguvu mpya na kuendelea na mapambano hayo.

Pamoja na hayo hali ilibadilika ghafla kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1970 ambapo dawa za asili na mpya zilianza kupata sura, mbinu ama njia mpya za matumizi pamoja na watumiaji wapya. Vijana wengi hasa mabarubaru **(wanawake na wanaume)** walianza kujifunza na hatimae kuwa wateja wazuri wa dawa hizo kwa malengo tofauti zaidi ikiwa ni **starehe**.

Matokeo yake hali ilianza kuvurugika na kutokuwa shwari katika maeneo mbali mbali humu duniani. Kwa ufupi athari na madhila ya kilimo, usafirishaji, usambazaji na matumizi ya dawa hizo haramu za kulevya yalianza kuonekana kila kona ya dunia hii.

**Ndugu Wananchi,**

Maadhimisho hayo huwa na kauli mbiu ama ujumbe maalum ambapo kwa mwaka huu ujumbe wetu ni **"People first: stop stigma and discrimination, strength prevention"** ambao unatafsirika kwa Kiswahili kwa maneno haya **"Utu kwanza, Acha unyanyapaa na ubaguzi imarisha kinga"** unaitaka jamii kuacha unyanyapaa kwa waathirika wa dawa za kulevya pamoja na kuzingatia usawa katika upatikanaji wa huduma zote za msingi kwa maisha na ustawi wa binaadamu.

**Ndugu Wananchi,**

Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kwa nafasi kushiriki kikamilifu katika kutoa taaluma kwa wenzetu wanajamii juu ya athari na madhila yote yale ya kiafya, kiuchumi na kijamii yatokanayo na janga hili pamoja na kuwasaidia waathirika wa dawa hizo kupata huduma za marekebisho ya tabia.

Ni dhahiri kuwa dawa za kulevya zina madhara tofauti katika mustakbali na maendeleo ya dunia. Sote kwa aina fulani ni wahanga wa tatizo hili kutokana na madhara yake yakiwemo yale ya vitendo vya wizi, vifo, ajali, magonjwa ya akili, magonjwa ya kujamiiana, ulemavu, kutokuwepo kwa amani na utulivu, mimba zisizotarajiwa, kubakwa, kulawitiwa na mengi mengineyo tunayojua.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa makisio duniani kuna watumiaji wa dawa za kulevya wanaopindukia milioni mia mbili na hamsini (Mil.250). Wengi wao ni

wale wa lile kundi la vijana wa umri kati ya miaka 15 hadi 30 tena zaidi na watu wanaopatikana katika miji mikubwa na maarufu humu duniani lakini kuongezeka kwa tatizo hili hata sehemu za mashamba biashara hii imeanza kushamiri hivi sasa.

Hapa Zanzibar napo hali si shwari kwani tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya linaendea kusumbua. Jumla ya watumiaji wa dawa za kulevya 9644 walisajiliwa katika vituo vya tiba na marekebisho ya kwa kipindi cha miaka 13, kati ya hao watumiaji 5063 (52%) wamerejea matumizi.

**Ndugu Wananchi**

Serkali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Hussein Mwinyi –Rais wa Zanzibar na MMwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imefungua Kituo Cha Tiba na Marekebisho ya Tabia (Rehabilitation Centre) kule KIDIMNI - wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. Jitihada za Mhe. Rais za kufungua kituo hicho zinalenga kuwapatia tiba na marekebisho ya tabia pamoja na mafunzo ya ujasiriamali waathirika wa matumizi ya dawa hizo. Tokea kituo hicho kufunguliwa Febuary, 2022 hadi sasa jumla ya vijana 252 walipokelewa katika kituo hicho, ambapo kati ya hao waraibu 21 (8.3%) wameachana na dawa za kulevya, waraibu 46 bado wanaendelea na huduma na wengine kushindwa kufanikiwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo utoro, kupata rufaa mental hospital na wengine kukatisha mkataba.

Aidha huduma hii pia hutolewa na taasisi binafsi kupitia Nyumba za Upataji Nafuu “SOBER HOUSES” ambazo kwa sasa zipo 4 (1 ipo

Pemba na 3 Unguja). Pia kupitia Wizara ya Afya waathirika wa dawa za kulevya wanapatiwa huduma ya tiba mbadala ya dawa ya METHADONE inayotolewa hapo katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili (MENTAL) iliopo Kidongo Chekundu. Karibu jumla ya watumiaji 1551 (wanaume 1471, wanawake 80) walisajiliwa katika kliniki hiyo kati ya hao watumiaji 39 (wanaume 36, wanawake 3) wamefanikiwa kuacha matumizi ya dawa za kulevya na watumiaji 926 (wanaume 881, wanawake 45) wanaendelea na huduma na kuhudhuria Kliniki kila siku.

**Ndugu Wananchi**

Juu ya yote hayo bado Zanzibar tunatajwa na kunyooshewa vidole kuwa ni moja ya njia kuu kimataifa inayotumiwa na wafanya biashara wa dawa za kulevya kwa **Ukanda huu wa Kusini**. Wafanyabiashara wa dawa hizo hasa HEROINE wanaitumia sana nchi yetu kama ni njia yao kuu katika harakati zao za kusafirisha mzigo wao kuelekea katika masoko huko Ulaya Magharibi na Marekani ya Kaskazini.

Jambo hili linatia doa jeusi haiba na sifa njema tulizorithi kutoka enzi na enzi kwa mababu zetu kimataifa. Mbaya zaidi inasababisha vijana wetu wanaotafuta ajira, kutokuajiriwa katika makampuni makubwa ya upakizi na upakuzi wa mizigo huko ughaibuni pamoja na mashirika ya meli hata kama sifa na vigezo wanavyo. Isitoshe hata hao

walioajiriwa na wale waajiriwa wapya wanakuwa katika uchunguzi mkubwa na mkali wa mara kwa mara.
Halikadhalika kuna taarifa za kusikitisha kwamba wengi wa wale wanaokamatwa na dawa za kulevya sehemu tofauti humu duniani ni vijana wa Kizanzibar. Baadhi yao hivi sasa wananyongwa ama wanasubiri kunyongwa katika mataifa tofauti na zaidi huko China, sasa suali ni kujiuliza nini kifanyike??

**Ndugu Wananchi,**
Lengo kuu la kuwa na siku hii ya kuadhimisha kupiga vita dawa za kulevya  si kusheherekea bali sote kwa umoja wetu na kila mmoja kwa nafasi yake duniani kutoa ushirikiano wa kutoa taarifa, kuandaa mbinu na mikakati mipya na iliyo imara ya kukabiliana ipasavyo na janga hili la dunia ili tulipunguze na kama itawezekana tulizike kabisa na ibaki kuwa historia kwa kizazi kijacho.

**Ndugu Wananchi,**
Janga la matumizi ya dawa za kulevya ni chanzo kikuu cha kuenea kwa kasi kwa yale maradhi thakili yanayojulikna duniani kote. Maradhi hayo ni pamoja na UKIMWI, Homa za INI aina ya B na C, maradhi ya moyo, figo na tatizo la ugonjwa wa akili. Ambapo huu ni mzigo mkubwa kwa jamii na taifa kuwa na jamii ambayo ni tegemezi kwa kila kitu na hasara kwa Taifa.

**Ndugu Wananchi,**

Namalizia maelezo yangu haya kwa kuwaomba tuipongeza kwa dhati Mamlaka ya Kudhibiti na Kuapambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na wadau wake wote waliomo kwenye mapambano hayo kwa jitihada zake mbali mbali inazozichukua za kutokomeza matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini. Sote tuwaunge mkono kwa kuwapa kila aina ya msaada ili kwa pamoja na kwa mashirikiano ya dhati tuweze kushinda vita hii na kubaki historia katika taifa hili. Kwa kumalizia nikushukuruni nyote kwa kunisikiliza na kuandaa kipindi hiki.

***"TUKISHIRIKIANA KWA PAMOJA ZANZIBAR BILA YA DAWA YA KULEVYA INAWEZEKANA"***

Ahsanteni sana.